

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Simu: 026-2322129
Nukushi: 026-2322126
Baruapepe: km@michezo.go.tz
Tovuti: www.michezo.go.tz



Mji wa Serikali-Mtumba,
2 Mtaa wa Michezo,
S. L. P 25,
40481 DODOMA

09 Aprili, 2025
Dodoma.

TAARIFA KWA UMMA

KUFUNGWA UWANJA WA BENJAMIN MKAPA KWA MUDA

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo inatangaza kuufunga uwanja wa Benjamin Mkapa kwa muda kuanzia leo tarehe 9 Aprili 2025 ili kupisha marekebisho ya eneo la kuchezea (Pitch) lililopata athari kubwa kufuatia mvua zilizonyesha na kufuatiwa na mchezo wa Robo Fainali wa Kombe la Shirikisho Barani Afrika kati ya Simba SC na Al Masry ya Misri.

Timu ya Wataalamu itanza mara moja kufanya tathmini ya kina ya madhara yaliyojitokeza na tarehe ya kufunguliwa kwa uwanja huo itatangazwa hapo baadaye.

Kufuatia uamuzi huu, timu zote ambazo zilipanga kuutumia uwanja wa Benjamin Mkapa zikiwemo zinazoshiriki mashindano ya Kimataifa zinaombwa kutafuta uwanja mbadala wakati Serikali ikifanya marekebisho ya eneo la kuchezea kwa dharura.

Wizara inaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza kutokana na kufungwa kwa uwanja huu kwa sasa.

Imetolewa na:
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO